



MEM

HABARI ZA
NISHATI & MADINI

Dawati la maoni ya Mhariri-Badra Masoud...Uk6

NewsBulletin

<http://www.mem.go.tz>

Toleo No.21

Limesambazwa kwa Taasisi na Idara zote MEM

Tarehe Juni 20-26, 2014

MGOGORO KATI YA MALAWI NA TANZANIA

Si kikwazo utafiti wa mafuta, gesi



Waziri wa Nishati
na Madini Profesa
Sospeter Muhongo

Kwa mfano kuna haya maeneo ya mipaka ambayo kuna rasilimali za gesi, mafuta na madini yanahitaji kasi na umakini mkubwa katika kufanya maamuzi ili kutokwamisha shughuli za utafiti wa mafuta, gesi na madini.

SOMA UK2

Gesi yazidi kugundulika Uk4 >> Bomba la gesi baharini lakamilika!! Uk10



OFISI YA MAWASILIANO SERIKALINI INAPOKEA HABARI ZA MATUKIO MBALIMBALI
KWA AJILI YA NEWS BULLETIN HII NA JARIDA LA WIZARA YA NISHATI NA MADINI

Wasiliana nasi Kitengo cha Mawasiliano kwa simu Namba +255 22 2110490 Fax 2110389 Mob: +255 732 999263
au Fika Ofisi ya Mawasiliano Ghorofa ya Tano (MEM) Barua pepe: badra77@yahoo.com

MIGODI MIKUBWA YALIPA BILIONI 527.8

Teresia Mhagama na Greyson Mwase

Wakala wa Ukaguzi wa Madini Nchini (TMAA) umeendelea kuibana migodi mikubwa ambapo jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 527.8 zimelipwa na migodi hiyo kama kodi ya mapato kwa kipindi cha mwaka 2009 hadi 2014.

Akizungumza kwenye maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam Afisa Habari wa Wakala huo Mhandisi Yisambi Shiwa alisema kuwa kutokana usimamizi imara wa Wakala huo kwa kushirikiana na taasisi nyingine za serikali kama Mamlaka ya Mapato nchini (TRA), Jeshi la Polisi n.k wakala huo umeendelea kuhakikisha kuwa migodi inalipa kodi stahiki kwa Serikali.

Mhandisi Shiwa aliongeza kuwa Wakala huo umeweka mikakati kabambe kuhakikisha kuwa makampuni ya madini yachangia ipasavyo katika mapato ya Serikali.

Akielezea mafanikio ya Wakala huo Mhandisi Shiwa alitaja mafanikio mengine kuwa ni pamoja na mapunjo ya kodi na tozo mbalimbali kulipwa serikalini na migodi baada ya kubainika kutolipwa ambapo kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2012 hadi Machi, 2014 jumla ya shilingi bilioni 8.89 zimelipwa na migodi mikubwa na ya kati kama mapunjo ya kodi na tozo mbalimbali zikijumuisha mrabaha, kodi ya zuio, ushuru wa huduma, SDL na PAYE.

Aliendelea kutaja mafanikio mengine kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa malipo ya mrabaha na kuongeza kuwa katika kipindi cha Juni, 2011 hadi Machi, 2014 Wakala umewezesha serikali kukusanya mrabaha wa jumla ya shilingi bilioni 3.6 kutokana na ukaguzi wa madini ya ujenzi na viwandani.

Mhandisi Shiwa alisema kiasi hiki ni kikubwa ikilinganishwa na kiasi kilichokuwa kinakusanywa kabla ya ukaguzi kuanza.

“Kwa mfano Ofisi ya Kanda ya Mashariki ilikuwa inakusanya wastani wa shilingi milioni tatu kwa mwaka kabla ya ukaguzi wa TMAA kuanza mnamo Julai, 2011.” Alisisitiza Mhandisi Shiwa.

Aliongeza kuwa Wakala huo umefanikiwa kudhibiti utorohwaji wa madini na ukwepaji wa mrabaha na kusisitiza kuwa tangu wakala uanze kukagua wasafirishaji wa mizigo katika viwanja vya ndege mwezi Julai, 2012 hadi Machi, 2014 jumla ya matukio 43 ya utorohaji wa madini yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 15.72 yameripotiwa katika viwanja vya ndege.

Mhandisi Shiwa alisisitiza kuwa kutokana na ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maeneo ya migodi, mazingira ya kazi yameboreshwa ambapo ajali za migodini zimepungua.



Baadhi ya wafanyakazi kutoka Wakala wa Ukaguzi wa Madini Nchini (TMAA) wakiwa katika maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, viwanja vya Mnazimmoja jiji Dar es Salaam

TUPO TAYARI KUTEKELEZA



Baadhi ya wawakilishi kutoka kampuni ya NOMAD wakimsikiliza kwa makini Waziri wa Nishati na Madini Profesa Sospeter Muhongo (hayupo pichani)

Mgogoro kati ya Malawi na Tanzania

Na Greyson Mwase

Waziri wa Nishati na Madini Profesa Sospeter Muhongo amesema kuwa mgogoro juu ya mpaka wa Ziwa Nyasa kati ya Nchi ya Tanzania na Malawi isiwe ni kikwazo katika shughuli za utafiti wa rasilimali za mafuta na gesi.

Profesa Muhongo alisema hayo mwishoni mwa wiki mara baada ya kusikiliza maelezo ya kampuni inayojishughulisha na shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi yenye makao yake makuu jijini London Uingereza ya NOMAD yenye nia ya kufanya utafiti wa mafuta na gesi katika Ziwa Nyasa.

Kampuni ya NOMAD ilijitambulisha na kuwasilisha taarifa na uzoefu wake katika shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi katika sehemu ambazo imewahi kufanya kwa nchi nyingine pamoja na nia yake ya kufanya utafiti katika Ziwa Nyasa mbele ya Profesa Muhongo,

wataalamu wa Wizara, pamoja na menejimenti ya Shirika la Maendeleo ya Petroli na Mafuta Nchini (TPDC).

Profesa Muhongo alisema kuwa sasa ni wakati wa nchi ya Tanzania kupitia wataalamu wake wa Shirika la

Kwa mfano mnaweza kutumia tafiti nyingi zilizofanywa na wanafunzi wa PhD wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Nairobi na makumbusho ya Royal Museum yaliyopo Brussels katika idara ya Jiolojia ambapo ninaamini kabisa mtapata taarifa nyingi za kijiolojia zitakazowawezesha kurahisisha utafiti wenu

TPDC kuchangamkia fursa za uwekezaji wa utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi kwa kufanya kazi kwa kasi hasa katika kufanya maamuzi lakini kwa umakini mkubwa.

“Kwa mfano kuna haya maeneo ya mipaka ambayo kuna rasilimali za gesi, mafuta na madini yanahitaji kasi na umakini mkubwa katika kufanya maamuzi ili kutokwamisha shughuli za utafiti wa mafuta, gesi na madini.

Profesa Muhongo aliongeza kuwa kutokufan-

ya maamuzi kwa wakati kwa sababu ya mgogoro wa maeneo ya mipakani ni kikwazo kikubwa cha maendeleo ya shughuli za utafiti wa rasilimali za gesi na mafuta.

Profesa Muhongo alisisitiza kuwa kinachotakiwa kufanyika ni

wataalamu wa Tanzania kukutana na wataalamu wa nchi husika na kukubaliana maeneo ya utafiti huku serikali ikiendelea na mazungumzo na nchi yenye mgogoro wa mpaka.

Profesa Muhongo aliendelea kusema kuwa Serikali ya Tanzania bado inaendelea na mazungumzo na Serikali ya Malawi na kuwataka wataalamu pamoja na kampuni ya NOMAD kuondoa hofu na kuendelea na shughuli za utafiti.

Aidha Profesa Muhongo aliipongeza

kampuni ya NOMAD kwa hatua yake ya kuwekeza kwenye utafiti kwenye Ziwa Nyasa na kutaka ipewe ushirikiano mkubwa.

Profesa Muhongo alitumia fursa hiyo kuishauri kampuni hiyo kuhusu maeneo ambayo inaweza kupata taarifa za awali zinazoweza kuiwezesha kupata mwanga wa kuanzia katika shughuli zake za utafiti.

“Kwa mfano mnaweza kutumia tafiti nyingi zilizofanywa na wanafunzi wa PhD wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Nairobi na makumbusho ya Royal Museum yaliyopo Brussels katika idara ya Jiolojia ambapo ninaamini kabisa mtapata taarifa nyingi za kijiolojia zitakazowawezesha kurahisisha utafiti wenu.” Alisisitiza Profesa Muhongo.

Profesa Muhongo aliongeza kuwa serikali ya Tanzania iko tayari kushirikiana na makampuni ya nje ya utafiti na uchimbaji wa gesi na mafuta ili kuhakikisha kuwa rasilimali zinagunduliwa na kuanza kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

KITWANGA: FIKIRIENI VYANZO VINGINE VYA UMEME

Na Asteria Muhozya, Mtera.

Naibu Waziri Nishati na Madini anayeshughulikia masuala ya Nishati Mhe. Charles Kitwanga amefanya ziara ya kutembelea Bwawa la kuzalisha Umeme la Mtera mwishoni mwa wiki kwa lengo la kuangalia mwenendo wa maji katika bwawa hilo.

Wakati akizungumza na watendaji wa Bwawa hilo, Kitwanga amewataka watendaji hao kuhakikisha kuwa Bwawa la Mtera linaendelea kuwa na kiasi cha maji ya kutosha wakati wote ili kuweza kuzali-

sha umeme wa kutosha.

“Lazima mhakikishe bwawa hili linakuwa na maji ya kutosha wakati wote. Hakikisheni kuwa vyanzo vya maji ya bwawa hili vinakuwa endelevu”. Ame-sisitiza Kitwanga.

Aidha, ameongeza kuwa, uzalishaji umeme kwa njia ya maji ni muhimu kutokana na gharama zake kuwa nafuu ikilinganishwa na gharama za kuzalisha umeme unaotokana na gesi au vyanzo vingine. Hivyo, amewataka wananchi wanaofanya shughuli zao jirani na vyanzo vya maji kuhakikisha wanavilinda kwa ajili ya maendeleo na manufaa ya taifa.

Katika hatua nyingine amewataka watendaji hao kufikiria vyanzo vingine vya kuzalisha umeme mbali na gesi badala ya kusubiri rasilimali ya gesi pekee kuweza kuzalisha umeme.

“Tukumbuke gesi inaweza kuisha, lakini kuna vyanzo vingine vingi ambavyo vinaweza kwenda sambamba na gesi, lazima tuwe wabunifu”. Ameongeza.

Aidha ameeleza kuwa, wananchi wana matarajio makubwa na nishati ya umeme hivyo, amewataka watumishi wa Wizara ya Nishati na Madini kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya kuwatumikia watan-zania huku wakitunguliza uzalendo.

Naibu Waziri Nishati Mhe. Charles Kitwanga akionyesha kipimo kinachotumika kuangalia kiwango cha maji katika bwawa la Umeme la Mtera



Mhandisi Mwandamizi masuala ya uendeshaji katika Bwawa la Mtera, Mhandisi Julius Chomora akimweleza Naibu Waziri Nishati Mhe. Charles Kitwanga namna mtambo wa uendeshaji umeme unavyofanya kazi. Anayefuatia ni Mhandisi Nishati Mwandamizi Wizara ya Nishati na Madini Salum Inegeja.

KAMPUNI ZA UZIDUAJI ZATAKIWA KUBOresha HUDUMA KWA JAMII

Na Veronica Simba – Dar es Salaam

Wawekezaji katika kampuni zinazojishughulisha na miradi ya uziduaaji nchini katika sekta za madini, gesi asilia na mafuta wameshauriwa kuingeza na kuboresha huduma kwa jamii hususan zinazozunguka miradi yao ili kujenga imani kwa jamii husika na hivyo kuleta mahusiano mazuri baina ya pande hizo mbili.

Rai hiyo imetolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Nishati na Madini anayeshughulikia Madini, Mhe. Stephen Masele wakati akizindua Jopo la Majaji wa Tuzo ya Rais ya huduma za jamii na uwezeshwaji kwa mwaka 2014.

Naibu Waziri Masele alisema kumekuwa na migogoro mingi baina ya wananchi wanaoishi jirani na miradi mbalimbali na wawekezaji wa miradi husika hali inayosababisha upotevu wa amani na kurudisha nyuma shughuli za kimaendeleo kwa pande zote.

Ameleza kuwa migogoro mingi inayotokea kwa kiasi kikubwa inasababishwa na wananchi kutokuwa na imani na wawekezaji kwa kuwa hawaoni faida inayotokana na uwepo wa miradi husika katika maeneo yao na badala yake wanaamini kuwa wawekezaji wakubwa wanawanyonya na kujilimbikizia wenyewe faida inayopatikana kutokana na miradi hiyo.

“Ni bahati mbaya kwamba, wawekezaji wengi siku hizi wanaamini wakishapata leseni ya kumiliki na kuendesha shughuli mbalimbali hususan katika sekta ya madini ambayo imekuwepo kwa muda mrefu sasa, ndiyo wamemaliza. Hawatambui umuhimu wa kuifanya jamii inayowazunguka itambue mchango wao,” alisema Masele.

Naibu Waziri alisisitiza kuwa migogoro iliyopo baina ya wananchi na wawekezaji itakwisha endapo wawekezaji wataweka nia ya dhati katika utoaji huduma zinazoridhisha kwa jamii.

Aidha, ameongeza kwamba endapo wananchi wataridhishwa na huduma zinazotolewa kwao na makampuni ya madini, gesi asilia na mafuta, kamwe hawatatamani wawekezaji hao waondoke nchini kama hali ilivyo sasa bali watakuwa wa kwanza kutetea uwepo wa wawekezaji hao.

Masele amewataka wawekezaji kutambua kuwa ufahamu wa wananchi kuhusu haki zao kwa sasa ni mkubwa tofauti na ilivyo-okuwa siku za nyuma na hivyo amewashauri wawekezaji kutoridhishwa na vibali au leseni za biashara wanazomiliki kisheria bali ni muhimu kuhakikisha wanapata kibali kutoka kwa jamii kuhusu shughuli wanazozifanya.

Tuzo ya Rais ya Huduma za Jamii na Uwezeshwaji kwa miradi ya Tasnia ya uziduaaji nchini hutolewa kila mwaka na ilitolewa kwa mara ya kwanza mwaka 2013. Kwa mwaka huu, tuzo husika inatarajiwa kutolewa mwishoni mwa mwezi Agosti.


Lengo la Tuzo hiyo ni kutambua mchango wa kampuni zinazojihusisha na miradi katika tasnia ya uziduaaji na kuhamasisha kampuni hizo kuingeza mchango wake katika maendeleo ya jamii hususan maeneo yanayozunguka miradi hiyo.

Neema gesi asilia

Na Teresa Mhagama

"Tunatarajia kuchimba visima zaidi na tunatumaini kuwa matokeo ya visima hivi yataongeza kiasi cha ujazo wa gesi asilia kwa ajili ya miundombinu ya mradi mkubwa wa gesi hapo baadaye na sasa eneo lingine la utafiti limeshaandaliwa na litajaribiwa ndani ya mwaka 2014 na 2015"

Ramani ya visima ambavyo ugunduzi wa gesi umepatikana Kitalu - 2



■Kiasi kikubwa chagundulika tena

Baada ya kampuni ya Ophir Energy Plc, wiki iliyopita kutangaza ugunduzi wa gesi asilia ambayo inaweza kuvunwa kwa futi za ujazo triloni 1.0 (1.0 tcf) katika kitalu namba 1 kwenye kisima cha Taachui kilichochimbwa katika kina cha urefu wa mita 4,215. Nayo kampuni ya utafiti na uchimbaji gesi asilia na mafuta ya Statoil na mshirika wake Exxon-Mobil wamegundua kiasi kingine kikubwa cha gesi asilia katika bahari ya Hindi nchini Tanzania.

Ugunduzi huu unahusisha kisima cha Piri-1 ambapo kiasi cha gesi asilia kilichopatikana kinakadiriwa kufikia triloni mbili mpaka tatu za ujazo.

Makamu wa Rais wa shughuli za utafiti za Statoil katika ukanda wa Magharibi, Nick Maden ameeleza kuwa ugunduzi huo unafanya jumla ya ujazo wa gesi iliyogundulika na washirika hawa kufikia takribani futi za ujazo triloni 20 kwenye kitalu namba 2

ambapo washirika hawa wanafanya shughuli za utafiti na uchimbaji

"Tangu mwaka 2012 tumekuwa tukipata mafanikio ya asilimia mia moja nchini Tanzania na eneo hilo limekuwa kitovu cha utafiti ndani ya muda mfupi sana. Ni kwa haraka tulitoka kwenye kuchimba kisima kimoja hadi kuwa na mkakati wa kuchimba visima vingi na Piri -1 ni muendeleo wa mafanikio haya," anaeleza Maden.

Ameleza kuwa ugunduzi huo mpya wa gesi asilia umefanyika katika eneo lenye kiwango kidogo cha mawe ya mchanga kama ilivokuwa wakati ilipogunduliwa gesi katika kisima cha Zafarani-1 kilichochimbwa mwaka 2012.

Makamu wa Rais huyo ameeleza kuwa ugunduzi katika kisima cha Piri-1 unakuwa wa sita katika safari ya ugunduzi katika kitalu namba 2 ikitanguliwa na ugunduzi mkubwa kwenye visima vya Zafarani-1, Lavani-1, Tangawizi-1, Mronge-1 na Lavani-2.

Ameleza kuwa uchimbaji katika kisima cha Piri -1 ambacho

kipo kilometa mbili kusini magharibi mwa kisima cha Lavani-1 kwa usawa wa mita 2,360 za kina cha maji ya Hindi ulifanywa na meli ya Discoverer Americas ambayo sasa imehama na inachimba kisima kingine cha Binzari katika kitalu namba 2 kwenye bahari hiyo.

"Tunatarajia kuchimba visima zaidi na tunatumaini kuwa matokeo ya visima hivi yataongeza kiasi cha ujazo wa gesi asilia kwa ajili ya miundombinu ya mradi mkubwa wa gesi hapo baadaye na sasa eneo lingine la utafiti limeshaandaliwa na litajaribiwa ndani ya mwaka 2014 na 2015" anasema Maden.

Kampuni ya Statoil inajihusisha na utafiti wa gesi asilia katika kitalu namba mbili ndani ya bahari ya Hindi kwa niaba ya Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC), kampuni hii ina hisa ya asilimia 65 katika kitalu hicho wakati mshirika wake ExxonMobil Exploration and Production Tanzania Limited wanamiliki hisa kwa asilimia 35.



Meli ya Discoverer America inayohusika na kuchoronga visima Kitalu 2 katika bahari ya Hindi Tanzania.

MUHIMU KUZINGATIA

UJUMBE WA WAZIRI WIKI HII

TUFANYE KAZI KWA UADILIFU, BIDII, WELEDI, NA USHIRIKIANO BILA KUKATA TAMAA

**DAIMA TUSONGE MBELE
KURUDI NYUMA NI MWIKO!!**



Tuzo za madini

Naibu Waziri wa Nishati na Madini anayeshughulikia Madini, Stephen Masele (Kulia) akimkabidhi Hadidu za Rejea Mwenyekiti wa Jopo la Majaji wa Tuzo ya Rais ya huduma za jamii na uwezeshwaji kwa miradi ya Tasnia ya uziduaji nchini, Prof. Samwel Wangwe.



Majaji tuzo ya Rais wapewa nyenzo za kazi

**Na Veronica Simba
Dar es Salaam**

Naibu Waziri wa Nishati na Madini anayeshughulikia Madini, Stephen Masele amezindua Jopo la Majaji wa Tuzo ya Rais ya huduma za jamii na uwezeshwaji kwa miradi ya Tasnia ya uziduaji nchini kwa kuwakabidhi Hadidu za Rejea watakazozitumia katika mchakato wa kuwapata washindi wa Tuzo husika.

Masele alizindua Jopo hilo linalotarajiwa kufanya mchakato wa kuwapata washindi kwa mwaka huu, mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na kuwataka Wajumbe wa Timu ya Majaji walioteuliwa, kufanya kazi hiyo kwa haki na umakini wa kutosha kwa maendeleo ya Taifa la Tanzania.

“Uteuzi wenu umezingatia umakini na kuaminika kwenu katika jamii, hivyo tunawatarajia muifanye kazi hiyo kwa weledi wa hali ya juu,” alisisitiza Naibu Waziri Masele.

Akizungumzia lengo la kuanzishwa kwa Tuzo husika, Masele alisema ni kuhamasisha utekelezaji wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na Sera ya ‘Local Con-

tent’ inayotaka kila kampuni inayojishughulisha na miradi ya uziduaji katika sekta za madini, gesi asilia na mafuta kuweka utaratibu wa kuwashirikisha wananchi walio karibu na miradi husika na wananchi kwa ujumla wake katika shughuli za maendeleo zinazochochewa na uwepo wa mradi.

Aidha, Naibu Waziri alisema Tuzo hiyo ya Rais inatarajiwa kuleta manufaa kwa Serikali, wawekezaji na jamii ya Watanzania wanaoishi karibu na miradi ya nishati na madini kwa kuchoea maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii kwa njia iliyo shirikishi na fungamanisho na sekta nyingine kiuchumi.

Aliongeza kuwa, tuzo hii itaharakisha kuwepo kwa fungamanisho kati ya sekta za nishati na madini na sekta nyingine za kiuchumi, pamoja na kuwepo kwa uwiano wa kutosha wa ukuaji wa sekta hizi; ikiwa ni pamoja na kuhamasisha, kuiwezesha na kuishirikisha jamii kwenye maeneo ya miradi ya nishati na madini katika kujikwamua kiuchumi na hivyo kupunguza umaskini.

Kwa upande wake, Kamishna wa Madini, Mhandisi Paul Masanja alitaja baadhi ya kazi za timu ya majaji kuwa ni pamoja na kutembelea maeneo ya miradi ya

tasnia ya uziduaji na kufanya tathmini na mahojiano na kampuni husika pamoja na wananchi wa maeneo hayo kwa uwazi ili kupima huduma za jamii zilizotolewa kwa kipindi cha mwaka 2013-14.

Kamishna Masanja alisema kazi nyingine ya majaji ni kukusanya taarifa za kampuni zinazowania Tuzo husika kwa ajili ya kuchambua na kuwapata washindi, kuangalia mifumo inayotumiwa na wawekezaji katika kubuni na kutoa huduma kwa jamii na kufanya tathmini ya ushirikishwaji wa Halmashauri za Wilaya na Serikali kuu katika huduma za jamii kwa wananchi.

Akizungumza kwa niaba ya majaji wenzake, Mwenyekiti wa Jopo hilo, Prof. Samwel Wangwe alitoa shukrani kwa kuaminiwa na ku-teuliwa kwao kuwa majaji wa zoezi hilo na akaahidi kuwa jopo la majaji wateule, litafanya kazi kwa weledi wa hali ya juu na kwa wakati, kama lilivyoelekezwa.

Miradi inayotegemewa kushiriki katika Tuzo ya Rais ya Huduma za Jamii na Uwezeshwaji kwa mwaka huu ni 98 ambapo 32 kati yake ni miradi ya utafutaji wa madini, 43 ni miradi ya uchimbaji madini na 13 ni miradi ya utafutaji na uchimbaji wa gesi na mafuta.



Kamishna wa Madini Mhandisi Paul Masanja, akitoa maelekezo kwa Majaji wa Tuzo ya Rais ya huduma za jamii na uwezeshwaji kwa miradi ya Tasnia ya uziduaji wakati wa uzinduzi wa Jopo hilo.

MEM
Mhariri

Dawati la Mhariri na Badra Masoud

Tumeweza na sasa
tunasonga mbele!!!

Ndugu wasomaji wa MEM News Bulletin napenda kuwakumbusha kwamba Kitengo changu cha Mawasiliano kilianzisha MEM News Bulletin mwezi Februari mwaka huu ambapo leo tumefikia toleo nambari 21 tangu kuanzishwa kwa jarida hili.

Ni wazi kuwa kila mwanzo wa jambo huwa na ugumu na changamoto zake, lakini kwetu sisi wakati tunaanzisha bulletin hii changamoto haikuwa kubwa zaidi ya upatikanaji wa taarifa lakini kadri siku zilivyokuwa zikisonga mbele hali ya upatikanaji wa taarifa uliboreka kutokana na wadau kuona umuhimu wa kutoa taarifa na kutushirikisha kwa kila jambo linaloendelea ndani ya Wizara na taasisi zake.

Lakini kikubwa napenda kumshukuru Kiongozi anayeongoza jahazi la Wizara yetu Komredi Prof. Sospeter Muhongo (Mb) kwa kutunga mkono na kututia moyo mara baada ya toleo la kwanza la Bulletin kutoka na zaidi alipotutaka tuisambaze bulletin hii kwa wingi na kwa watu wengi zaidi huku yeye mweyewe akiwa mstari wa mbele kulipigia debe gazeti letu hadi mezani kwa Mhe. Rais Dk. Jakaya Kikwete na Waziri Mkuu Mhe. Mizengo Pinda pamoja na viongozi wengine.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Naibu Mawaziri Mpambanaji Mhe. Stephen Masele (Mb) na Mhe. Charles Mhangwa Kitwanga "mawe matatu" kwa ushirikiano mkubwa na wenye kutia moyo.

Naye Kamanda Mpiganaji Eliakim Maswi, Katibu Mkuu, alinipa "surprise" kubwa baada ya toleo la kwanza kuchapishwa kwani sikutarajia kama angelifurahia hivyo, lakini kwa kweli alifurahi sana na kuahidi kutoa ushirikiano kwa Kitengo changu bila kuchoka na alinipa moyo kwa kuniambia "Mama chapa kazi, mimi kama KM nitakupa ushirikiano" kwa kweli nilifarjika sana. Tunamshukuru sana KM kwa ushirikiano wake na kwa kutuwezeshia ili tufanye kazi kwa ufanisi.

Sijawasahau Viongozi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara ambao nao wana mchango mkubwa sana katika maendeleo ya Bulletin hii wakiwemo Makamishna wote, Wakuu wa Idara, Vitengo, Wakurugenzi wa Mashirika, wafanyakazi wote wa Wizara na taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao mzuri na wa kutia moyo.

Kutokana na ushirikiano mliotupa tangu tulivyoanzisha Bulletin hii nimeona kumbe tunaweza kwani uwezo tunao, nguvu tunazo na nia tunayo ya kufanya vizuri hasa ikizingatiwa ushirikiano wa kutosha tunapewa jambo lililolisukuma nifanye mabadiliko kidogo kwenye Bulletin hii ili iwe na muonekano mpya au sura mpya na kuongeza baadhi ya vitu ikiwemo maoni ya Mhariri ambaye ni mimi mwenyewe na ambayo yatatoka ya kila wiki.

Nimeamua kubadili muonekano huo mpya kwa kuwa gazeti hili kwa sasa linasomwa na watu wengi mbalimbali wakiwemo wa Wizara, taasisi mbalimbali za Serikali, binafsi na mitandao ya kijamii hivyo limekuwa na wigo mpana katika jamii.

Kwa kawaida maoni haya yatakuwa yakigusa masuala mbalimbali ambayo tutakuwa tunayasikia kutoka kwa jamii na yanayohitaji kufanywa kazi ili kuiepusha Wizara kuwa na taswira mbaya.

Ninaomba ieleweke kwamba, yale yote nitakayoandika kwenye safu hii hayana uhusiano wowote wala nia ya kumchafua mtu, Idara, Kitengo ama taasisi bali lengo lake ni kujenga pamoja na kupaka rangi nyeupe dhidi ya wabomoaji, wapotoshaji na wanaoichafua Wizara yetu kwa kuipaka matope. Kamwe hatutakubali hilo lifanyike.

Ninaomba ushirikiano mkubwa kwa kila mmoja wetu kwa kuanza nawaomba Maofisa Habari wenzangu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kuhakikisha kwamba MEM news bulletin mnaibandika na kuwatumia Viongozi na Wafanyakazi wote wa taasisi zenu.

Tukumbuke kwamba bulletin hii inatuhusu wote kwani habari zinachapishwa zinatoka Wizarani pamoja na taasisi zote zilizo chini ya Wizara hivyo hamna sababu yoyote ya Msingi ya kutoibandika katika mbao za matangazo kwenye ofisi zenu.

Naomba tushirikiane pamoja kujenga Wizara yetu ili tutekeleze majukumu yetu kwa ufanisi kwa kuwatumikia Watanzania.

Daima tuijenge Wizara yetu kwa ufanisi!!!!

TANSORT YAPANDA CHATI

Na Veronica Simba

Kitengo cha Uthamini wa Almasi na Madini ya Vito (TANSORT) cha Wizara ya Nishati na Madini, kimefanikiwa kuboresha tasnia ya almasi nchini hadi kufikia kiwango cha kimataifa.

Hayo yamesemwa jana na mtaalamu wa almasi na madini ya vito vya rangi kutoka kitengo hicho, Teddy Goliamu (pichani kulia) wakati akitoa maelezo kwa mteja aliyetembelea Banda la Wizara ya Nishati na Madini katika Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayoendelea katika Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

Mtaalamu huyo ametaja mafanikio ya TANSORT kuwa ni pamoja na kuongezeka kwa mrabaha unaokusanywa na Serikali pamoja na kuongezeka kwa wastani wa bei za almasi na madini ya vito yanayozalishwa hapa nchini.

Ameongeza kwamba TANSORT imefanikiwa kulinda mapato ya Serikali kwa kutoa miongozo ya bei za almasi na madini ya vito na pia wigo wa shughuli za Kitengo umeongezeka kwa kuanza kuwahudumia wazalishaji na wafanyabiashara katika ofisi za madini Arusha, Dar es Salaam, Shinyanga na Songea.

Akizungumzia mipango endelevu ya Kitengo hicho, Bi Goliamu alisema ni pamoja na kuandaa miundombinu na kutengeneza mazingira salama ya biashara ya vito nchini, kue-



"Huduma za uchambuzi na uthamini (sorting) wa madini ya almasi kwa sasa unafanyika hapa nchini badala ya Uingereza kama ilivyokuwa hapo awali hivyo nawashauri wadau wetu wasisite kututembelea ili kupata huduma zetu," alisisitiza

ndelea kutoa mafunzo kwa wadau wa tasnia ya almasi na vito pamoja na kuendelea kusimamia vema tasnia husika.

Mtaalamu huyo amewataka wananchi wote wanaohitaji huduma za TANSORT hususan

wadau wa tasnia ya almasi na vito kukitumia vema Kitengo hicho kwani kinao wataalamu wa kutosha walioboea katika fani husika.

"Huduma za uchambuzi na uthamini (sorting) wa madini ya almasi kwa sasa unafanyika hapa nchini badala ya Uingereza kama ilivyokuwa hapo awali hivyo nawashauri wadau wetu wasisite kututembelea ili kupata huduma zetu," alisisitiza Teddy.

Kitengo cha TANSORT kilianzishwa mwaka 1966 chini ya Wizara ya Nishati na Madini kikiwa na malengo makuu mawili; kusimamia na kuhakikisha kwamba mrabaha stahiki unakusanywa na kulipwa serikalini na pia kuhakikisha almasi na madini ya vito yanayozalishwa hapa nchini yanapata bei bora.

Baadhi ya majukumu ya Kitengo hicho ni kuthamini almasi na madini ya vito kwa lengo la kukokotoa mrabaha, kutayarisha miongozo ya bei za madini zinazotumika kukokotoa mrabaha, kutoa huduma za kijemolojia kwa wachimbaji wadogo na wa kati pamoja na kusimamia mauzo ya almasi na madini ya vito ndani na nje ya nchi.

Majukumu mengine ni kutoa huduma ya ushauri wa masoko, ukataji na ukadiraji thamani kwa wachimbaji wadogo na wa kati, kufanya utafiti wa masoko na bei za almasi na madini ya vito, kutunza takwimu za uzalishaji na mauzo ya almasi na madini ya vito pamoja na kusimamia tasnia ya almasi na madini ya vito nchini.

KWA HABARI PIGA SIMU
KITENGO CHA MAWASILIANO

TEL-2110490
FAX-2110389
MOB-0732999263

BODI YA UHARIRI

MHARIRI MKUU: Badra Masoud
MSANIFU: Essy Ogunde
WAANDISHI: Veronica Simba, Asteria Muhozya, Greyson Mwase
Teresia Mhagama, Nuru Mwasampeta

FIVE
PILLARS OF
REFORMS

INCREASE EFFICIENCY

QUALITY DELIVERY
OF GOODS/SERVICESATISFICATION OF
THE CLIENTSATISFICATION OF
BUSINESS PARTNERSSATISFICATION OF
SHAREHOLDERS

Kutoka Mnazimmoja

<http://www.mem.go.tz>

WIKI YA UTUMISHI WA UMMA



Mhandisi Mwandamizi Masoko
na Huduma kwa Wateja , Juliana
Pallangyo kutoka Shirika la Umeme
Tanzania (TANESCO) akitoa
ufafanuzi kuhusu namna Shirika
hilo linavyofanya kazi kwa baadhi ya
wanafunzi waliotembelea banda la
Taasisi hiyo.



Wafanyakazi, Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zake (TANESCO, STAMICO, MRI, TPDC, na TMAA) wakipita mbele ya mgeni rasmi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Utawala Bora, George Mkuchika (hayupo pichani) wakati wa ufunguzi rasmi kwa Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.



Kamishna Msaidizi wa Madini, Uratibu, Mhandisi John Shija (Wa kwanza kushoto) akifuatilia maelezo yanayotolewa na Mtaalamu wa madini ya Vito vya Rangi na Almas Bibi Teddy Goliama (katikati) anayewaeleza wanafunzi aina mbalimbali za madini yanayopatikana Tanzania walipotembelea Banda la Wizara.



Baadhi ya wafanyakazi kutoka Wizara ya Nishati na Madini na Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC) wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu sekta za Nishati na Madini.

WIKI YA UTUMISHI WA UMMA



Watumishi wa Wizara ya Nishati na Madini na baadhi ya Watumishi wa Taasisi zilizo chini yake wakiwa katika picha ya pamoja katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika Viwanja vya Mnazi Mmoja Jijini Dar es Salaam.



Mtaalam kutoka Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (SMMRP), Getty Massawe (kushoto) akielezea jinsi mradi huo unavyochangia katika kukuza sekta ya madini na kuiboresha kwa manufaa ya nchi.



"Elimu kwa Umma". Msemaji wa Wizara ya Nishati na Madini, Badra Masoud akizungumza na waandishi wa habari kuhusu juhudi zinazofanywa na Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zake katika kuendeleza rasilimali inazozisimamia.



Watumishi wa Wizara ya Nishati na Madini, Juma Mkobya kutoka Mradi wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) (wa kwanza kulia) na Mhandisi Robert Dule (katikati) wakimskiliza mmoja wa wageni aliyetembelea Banda la Wizara wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma.



Mtaalam kutoka Kitengo cha Uthaminishaji wa Almasi na Madini ya Vito (TANSORT), Teddy Goliama akimweleza mwananchi kuhusu huduma zinazotolewa na kitengo hicho kwa lengo la kukokotoa mrabaha wa madini hayo.



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO Mhandisi Edwin Ngonyani katika kikao na waandishi wa Habari (hawapo pichani) jijini Dar es Salaam.

STAMICO kuipatia serikali gawio

**NA LEONARD
MWAKALEBELA,
STAMICO**

Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) linatarajia kuanza kuipatia serikali gawio kutokana na miradi yake mbalimbali ndani ya kipindi cha miaka miwili au mitatu ijayo.

Aidha STAMICO imetangaza kuji-panga upya na kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa kuwapatia mafunzo, utaalamu, zana za uchimbaji madini pamoja na kuwasaidia kupata soko na mikopo kutoka katika taasisi za fedha.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi

Mtendaji wa STAMICO Mhandisi Edwin Ngonyani amesema gawio hilo litapatikana kutoka katika miradi mitano ya Shirika ambayo ipo tayari kuanza ikiwemo ile itakayosimamiwa kwa asilimia mia moja na STAMICO na ile ya ushirikiano na wawekezaji.

Mhandisi Ngonyani alisema mkakati wake mkubwa ni kuhakikisha kuwa STAMICO inajiendesha kwa faida na kupeleka fedha Hazina badala ya kutegemea fedha za ruzuku kutoka Serikalini kuliendesha Shirika.

“Nimeanza kazi hapa Juni Mosi mwaka huu, kazi zangu kuu ni mbili, moja ni kuhakikisha shirika linapeleka fedha Hazina, hii tabia ya mashirika ya umma ya kuchukua fedha hazina itakoma kwa shirika hili, na mbili kuwasaidia wachimbaji wa-

dogo” alifanua Mhandisi Ngonyani.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji huyo amesema anachotaka ni kuwafanya wachimbaji wadogo wa madini nchini wawe sehemu ya wawekezaji, kama ambavyo wawekezaji wa nje wanavyoweza kwa kutotegemea fedha zao za mifukoni bali mikopo kutoka katika taasisi za fedha, ndivyo ambavyo STAMICO pia itakavyowawezesha wachimbaji wadogo kunufaika na mikopo kutoka katika mabanki mbalimbali.

Alisema hilo litawezekana baada ya mkakati wa STAMICO wa kuanzisha na kuboresha taarifa za wachimbaji wadogo kukamilika ambapo taarifa hizo zitainishwa mahali walipo, aina ya madini wanayochimba na mahitaji yao.

“Tutahakikisha Watanzania wanapata

fursa ya uwekezaji na kuwasaidia wachimbaji wadogo waweze kuchimba madini kwa faida,” alisisitiza Mhandisi Ngonyani.

Naye Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa STAMICO, Bw. Peter Gembe alisema kupitia mradi wa Kiwira, Shirika linalenga kuzalisha megawati sita hadi 200 zitakazoringizwa kwenye Gridi ya Taifa kupitia njia ya kusafirisha umeme yenye urefu wa kilomita 100.

Bw Gembe alisema serikali imewakabidhi rasmi nyaraka na mikataba kwa ajili ya kuendesha mgodi wa Kiwira ili taratibu zinazofuata za utekezaji ziweze kufanyika.

Alisema STAMICO ina mpango wa kupanua mgodi chini ya ardhi na wanahitaji kufungua mgodi wa wazi ili kuweza kuzalisha tani milioni 1.5 za makaa ya mawe.

TANZANIA DAIMA LAIKOSEA WIZARA Kuburuzwa Mahakamani

■Wembe ni uleule ■Itaje Kampuni iliyofadhili kongamano viongozi wa dini

Na Mwandishi Wetu

Baada ya Baraza la Habari Tanzania (MCT), kusikiliza shauri la Wizara ya Nishati na Madini (MEM) dhidi ya gazeti la Tanzania Daima imebaini kwamba ilikiuka maadili ya uandishi wa habari kwa kuandika habari iliyogemea upande mmoja yenye uvumi na iliyosheheni maoni ya mwandishi wa habari hivyo sasa MEM imeamua kwenda Mahakamani.

Wizara ya Nishati na Madini iliwasilisha malalamiko hayo MCT dhidi ya gazeti la Tanzania Daima kutokana na habari iliyoandikwa na gazeti hilo Mei 16, 2014 yenye kichwa cha habari "Kashfa mpya Nishati na Madini".

Habari hiyo ilidai kwamba Wizara ya Nishati na Madini imejikuta ikiingia katika kashfa nyingine baada ya kudaiwa kufadhiliwa katika maandalizi ya kongamano lake la viongozi wa dini lililofanyika katika hoteli ya Whitesands hivi karibuni na moja ya Makampuni yaliyopewa leseni ya kutafiti na kuchimba gesi nchini.

Aidha, taarifa hiyo iliendelea kudai kwamba kampuni hiyo ni moja ya makampuni makubwa yanayopigwa chapuo na Mhe. Waziri Muhongo na kuongeza kuwa Kampuni hiyo ya utafiti na uchimbaji gesi na mafuta ililipia gharama za malazi kwa viongozi zaidi ya 200 ambapo kila mjumbe alilipwa dola za Marekani 180 (sawa na sh. 300,000) kwa siku, gharama za kujikimu sh. 200,000 na tiketi za ndege kwa wajumbe walioko nje ya jiji la Dar es Salaam.

Vilevile, gazeti hilo lilidai kwamba, baadhi ya wajumbe wenye misimamo mikali walimwagiwa fedha kuzungumzia dhana ya wawekezaji wa ndani kutokuwa na uwezo wa kuwekeza kwenye sekta ya gesi.



Baada ya Kamati ya Maadili ya MCT kusikiliza pande zote mbili Juni 16, 2014 imebaini kwamba kumekuwapo na mapungufu makubwa katika habari hiyo kutokana na habari hiyo kuegemea katika uvumi badala ya ukweli uliothibitishwa.

Aidha, Kamati hiyo ilisema kwamba hata chanzo cha tuhuma zenyewe zilizoandikwa kilikiri kuwa tuhuma hizo zilikuwa ni uvumi na kwamba uvumi huo ulijibiwa na upande wa pili na Waziri wa Nishati na Madini hivyo Tanzania Daima haikuwa na sababu ya kuandika uvumi huo.

Kamati pia ilibaini kwamba Wizara ya Nishati na Madini ilipewa fursa na kujibu uvumi huo ambapo Waziri wa Nishati na Madini alikanusha habari hiyo lakini mwandishi aliendelea kuandika habari hiyo kwa mtindo wa kuegemea upande mmoja huku mwandishi akiweka maoni yake ndani ya hilo jambo ambalo ni kinyume cha maadili na miiko ya uandishi wa habari.

Kamati hiyo ya Maadili ilibaini kwamba habari

iliyochapishwa haikuwa ya mwendeleo (running story) kama Mhariri wa gazeti hilo alivyodai mbele ya Kamati hiyo. Hata kama ingekuwa ni taarifa ya mwendeleo hiyo isingemaanisha kuchapisha taarifa isiyokamilika au iliyokuwa na uvumi.

Pamoja na tuhuma zilizotolewa ndani ya habari iliyochapishwa, Kamati ya Maadili iliona kwamba Wizara ya Nishati na Madini ilipaswa kujibu tuhuma hizo kwa lengo la kutoa taarifa sahihi kwa umma ambayo ni hayo ya msingi.

Baada ya kubaini kwamba gazeti la Tanzania Daima limekiuka maadili na miiko ya uandishi wa habari kwa

kuandika habari ya uvumi na isiyokuwa na ukweli wowote na kuonekana kwamba walikuwa na hila dhidi ya viongozi wa Wizara, Kamati hiyo iliagiza gazeti hilo liombe radhi ukurasa wa tatu (3) ndani ya siku saba tangu tarehe ya uamuzi wa Kamati ya Maadili.

Kamati hiyo pia iliagiza kuwa Tanzania Daima lifanye mahojiano na Wizara ya Nishati na Madini kuhusu masuala yaliyoandikwa katika habari inayoalalamikiwa pamoja na masuala mengine muhimu ambayo gazeti na Wizara wataona yana umuhimu na kuchapisha taarifa inayotokana na mahojiano hayo ndani ya siku 21 kutoka siku ya uamuzi wa Kamati hiyo.

Hata hivyo, Wizara ya Nishati na Madini haikukubaliana na uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Baraza la Habari Tanzania kwani madhara yaliyotokea baada ya habari hiyo kuandikwa ni makubwa na hayawezi kutatuliwa hivyo Wizara imeamua kuliwasilisha shauri hilo mahakamani.

Ujenzi bomba la gesi baharini wakamilika!!

Na Malik Munisi

Ujenzi wa bomba la gesi lenye urefu wa kilomita 25.657 lililokuwa likijengwa katika bahari ya Hindi nchini Tanzania umekamilika kwa asilimia 100%.

Mtaalam kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, (TPDC), Baltazar Mrosso amesema kuwa bomba hilo lenye kipenyo cha inchi 24 litaibukia katika eneo la SomangaFungu ambapo litaungana na bomba kubwa litakalofirisha gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam.

Amesema kuwa Utekelezaji wa mradi huo wa ujenzi wa bomba la gesi baharini ulikuwa unaenda sambamba na kutoboa njia ya bomba kwenye barabara, kazi amimeshakamilika kwa asilimia kubwa

kwani tayari njia 25 kati ya 26 zimefanywa kazi.

Vilevile ameeleza kuwa ujenzi wa bomba litakalofirisha gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam unaendelea kwa kasi kubwa.

Mtaalam huyo kutoka TPDC amesema kuwa hadi mwezi Mei mwaka huu tayari mabomba yapatayo 451 yalikuwa yameshasafirisha kutoka maeneo ya kuhifadhi kuelekea maeneo ya ujenzi kwa ajili ya kuyaunganisha.

Ameleza kuwa tayari kilometa 420 za mabomba haya yameshapangwa katika mstari mmoja na kuyaunganisha katika maeneo ya nchi kavu.

Mrosso amesema kuwa hadi mwezi Mei mwaka huu, uchimbaji wa njia ya kulaza mabomba haya wenye kilomita 263

ulishafanyika hii ikiwa ni asilimia 52.19% ya utekelezaji wa uchimbaji.

Mhandisi Mrosso aliongeza kuwa tayari kilomita 200 za bomba hili zimeshawekwa katika njia yake sambamba na mkongo wa mawasiliano ambao utawezesha usafirishwaji wa taarifa endapo kuna tokea uvujaji wa gesi au aina yeyote ya hali isiyokuwa ya kawaida.

Kuhusu ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika maeneo ya Madimba na Songosongo sehemu ambazo viwanda vya kuchakata gesi asilia vitajengwa, Mrosso ameeleza kuwa ujenzi wa nyumba hizi za kisasa umekamilika kwa asilimia 94.47% kwa upande wa Madimba na asilimia 86.64% kwa upande wa Songo Songo.



Bomba la gesi

WIZARA YA NISHATI NA MADINI

Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Wasiliana nasi kwa simu Namba +255 22 2110490 Fax 2110389 Mob: +255 732 999263 au Fika Ofisi ya Mawasiliano Ghorofa ya Tano (MEM) Barua pepe: badra77@yahoo.com

